KATIKA MAHAKAMA KUU ZANZIBAR
IMESIKILIZWA VUGA
KESI YA MADAI RUFAA NO. 9 YA 2012
KUTOKA KESI YA MADAI YA RUFAA NO. 24/2011
KUTOKANA NA KESI YA MADAI NO. 24/2011 MAHAKAMA YA KADHI WA RUFAA VUGA

1. **ZULEKHA MAULID SULTAN**
2. **SHARIFA ABDALLA IDDI ..... WAOMBA RUFAA**
3. **SALUM HASSAN SALMIN**

DHIDI YA

1. **MAKAME MASLAHI MAKAME**
2. **ZAMZAM TALIB ALI**
3. **KHADIJA ABDALLA ..... WAPINGA RUFAA**
4. **KATIBU MTENDAJI**
   KAMISHENI YA WAKFU
   NA MALI YA AMANA

H U K U M U

Omar Makungu, Jaji Mkuu

Hukumu hii ni matokeo ya rufaa iliyowasilishwa na Waomba rufaa katika kesi hii kupinga hukumu iliyotolewa na Naibu Kadhi Mkuu tarehe 16/02/2012.

Waomba rufaa katika rufaa hii wamewasilisha sababu 5 za rufaa kwa ajili ya mazingatio ya Mahkama. Sababu hizo ni kama zifuatazo :

1. Kwamba, Naibu Kadhi Mkuu amekosea kisheria na kushindwa kuchanganua kinachodaiwa katika rufaa iliyopelekwa mbele yake na ameshindwa kisheria kutoa ufafanuzi wa kuwa dai lililofunguliwa halikupaswa kisheria kusikilizwa na Mahkama ya Kadhi.

2. Kwamba Naibu Kadhi Mkuu huyo msomi ameshindwa kisheria kutambua kuwa katika eneo hilo la jengo la Tamtam Bar kuna maeneo binafsi yanayomilikiwa na Waomba rufaa pamoja na kuwa maeneo hayo yamezunguushiwa ukuta.

3. Kwamba, Naibu Kadhi Mkuu huyo msomi amekosea kisheria kwa kauli yake ya maandishi aliyotaka jengo la Tamtam Bar liuzwe na kinachopatikana kigaiwe kwa kufuata taratibu za Kiislamu bila ya kuzingatia kuwa jengo hilo linatumika kwa kuuzia pombe ambapo kwa mujibu wa sheria za kiislamu imeharamishwa, hivyo ni wazi kuwa chochote kitakachotumiwa baada ya kuuzwa kwa bar hiyo hakitakuwa halali.

4. Kwamba, Naibu Kadhi Mkuu huyo msomi amekosea kisheria kufuata maelekezo ya Kadhi wa Wilaya kuhusiana na mauzo ya eneo hilo kati ya Marehemu Mama wa Waomba rufaa na Waombewa rufaa na ameshindwa kuzingatia kuwa maeneo hayo hayakuuzwa na Mama wa waomba rufaa isipokuwa yameuzwa na watu mbali mbali kama vielelezo vilivyoelekeza ambavyo Mahakama haikuvizingatia.

5. Kwamba, hata ingelikuwa Waomba rufaa wameandikiwa, Marehemu alikuwa na haki ya kufanya hivyo kwa kuzingatia kuwa hadi Marehemu anakata roho hakuwa akizungumza na Mpingarufaa Nam. 1 na 3 (walikuwa hawasemi). Kutokana na sababu hizo wameomba Mahakama hii kukubali rufaa yao na kutengua maamuzi ya Naibu Kadhi Mkuu.

Kwa upande wa Wapinga rufaa nam. 1 hadi 3 wamepinga rufaa hiyo kwa kuwa haina msingi na kuomba Mahkama iitupilie mbali. Kwa upande wa Mpinga rufaa Nam. 4 yeye hakuwa na cha kusema ila kungojea maamuzi ya Mahakama katika shauri hili. Mahkama hii baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili haina budi kuzizingatia na kuzichambua hoja hizo na baadae kutoa maamuzi. Kabla ya

kufanya hivyo ni vyema kunukuu hapa hukumu ya Naibu Kadhi Mkuu ambayo linajieleza kama ifuatavyo:

"Mahkama baada ya kuyaona hayo imetoa hukumu ifuatayo:"

(a) Eneo lote la jengo la Tamtam Bar liuzwe na baada ya kuuzwa fedha zitakazopatokana zitumike kwa kufuata taratibu za kisheria ya Kiislamu ikiwemo:

- Kulipa madeni
- Kutolewa Wasia usiozidi thuluthi ya mali
- Kuwarithisha wanaostahiki kurithi.

Baada ya kusikiliza hoja za pande mbili katika rufaa hii, Mahkama pia ilitembelea eneo la mzozo tarehe 26/06/2012 na kupata nafasi ya kuliona eneo lenyewe lenye mzozo pamoja na kupata maelezo ya Katibu wa Sheha na Bw. Mussa Kheri Ali muuzaji wa eneo husika

Maelezo yaliyotolewa na Katibu wa Sheha hayana tofauti na yale yaliyotolewa na Sheha mwenyewe Bw. Kombo Mkuni Ali mbele ya Mahakama ya Kadhi wa Wilaya.

Aidha, maelezo yaliyotolewa na muuzaji mbele ya Mahkama hii pia yanaendana na maelezo aliyoyatoa mbele ya Mahkama ya Kadhi wa Wilaya.

Baada ya kuliona eneo la mzozo na baada ya kupata maelezo ya ziada ya Katibu wa Sheha na muuzaji na baada ya kupitia upya mwenendo wa kesi ya msingi katika Mahakama ya Kadhi wa Wilaya, Mahakama hii imeona kuwa kuna ushahidi wa nyaraka zilizowasilishwa ambazo ni kielelezo ZSS VII ni mauzo kati ya Bw. Mussa Kheri Ali na Bi Sharifa Abdalla Iddi, Zulekha Maulid na Salum Hassan Salmini, Waraka huu ambao ni wa kiwanja kimoja wapo haukumuhusisha Bi. Hawa Iddi. Aidha kiambatisho ZSS IX ya mauziano ya kiwanja baina ya Mussa Kheri Ali na Bi Sharifa Abdalla Iddi. Mauziano ya viwanja viwili hivi havihumuhisishi kabisa Bi. Hawa.

Aidha Mahakama hii baada ya kuupitia kwa makini ushahidi wa Sheha wa Nungwi uliotolewa katika Mahkama ya Kadhi wa Wilaya, Mahakama

imebaini kuwa Bi Hawa amekiuza kiwanjwa kinachodaiwa amekinunua yeye kwa pesa zake na kujenga.

Ushahidi wa Sheha wa Nungwi Bw. Kombo Mkuni unasomeka kama ifuatavyo:

"Ninavyofahamu mwaka 2010 alikuja Bi Shori akataka tuzungumze tukakaa akaniambia hivi sasa anaumwa na sina chochote cha kunisaidia, nikamuuliza kwani huna kitu akasema ndio mana nataka niuze eneo langu, jee unataka umuuzie nani? akasema siwezi kumuuzia mtu mbali nitawauzia wanangu wanaotafuta pesa nikamwambia walete hao watoto. Alikuja nao na tukatoka mpaka hapo penye eneo lenyewe ambalo limegawika sehemu mbili sehemu ambayo imeshauzwa ni sehemu inayofanyiwa biashara silo lakini ninaliuza ni lile ambayo haijajengwa nitawauzia watoto wangu watatu watoto wenyewe ni (1) Sharifa (2) Zulekha na (3) Salum. Hapo mimi nikaanza taratibu zangu tukaenda Ofisini tukaandika maandishi yaliandikwa na Katibu wangu hapo sikuwa na jengine hayo ndio ninayoyafahamu."

Mahkama hii baada ya kuzingatia ushahidi huu ambao umetolewa kwa kula kiapo imetuthibitikia kuwa kiwanja kimoja kimenunuliwa na Waomba rufaa

kwa Bw. Mussa Kheri Ali na chengine Waomba rufaa wameuziwa na Mama yao Bi Hawa ingawa katika Mkataba imeandikwa Bw. Mussa Kheri. Mahkama hii imeridhika kutokana na maelezo yaliyotolewa na Muuzaji kuwa waliamua baadae viwanja hivyo kuvichanganya na kuwa kimoja ingawa vimeauzwa tafauti na alifanya hivyo baada ya kuambiwa na Bi. Hawa mwenyewe kwa kuwa Waomba rufaa ndio aliokuwa akifanya nao biashara.

Baada ya uchambuzi huo, Mahakama hii imeridhika na sababu za rufaa na maelezo yaliyotolewa na hivyo kuwa na maoni sehemu ya Tamtam Bar sio katika mali za Marehemu Bi. Hawa zinazotaka kurithiwa. Tamtam Bar ambayo iko katika viwanja viwili vilivyogeuzwa kimoja ni mali ya Waomba rufaa.

Kwa hivyo, Mahkama hii inatengua uamuzi na hukumu iliyotolewa na Naibu Kadhi Mkuu kuwa sehemu hiyo iuzwe na irithiwe. Tamtam Bar sio mali ya kurithiwa bali ni mali ya Waomba rufaa. Mali ya Marehemu ni ile sehemu yenye vyumba vya kulala ambayo haina ugomvi kwa maoni yetu. Hii ndio Hukumu ya Mahkama hii.

Sgd: Omar O. Makungu Jaji Mkuu

12/07/2012

Masheikh:

1. **Sheikh Uwesu Machano**
2. **Sheikh Juma Faki Choum**
3. **Sheikh Kani Mkanga**
4. **Sheikh Fadhil Pandu Pandu**

Mahkama : Hukumu hii imesomwa mbele ya Waomba rufaa na Wapinga rufaa.

Sgd: Omar O. Makungu Jaji Mkuu

12/07/2012

Nathibitisha kuwa hii ni nakala sahihi ya hati ya asili.

Sgd. GEORGE J. KAZI

MRAJIS,

MAHAKAMA KUU – ZANZIBAR.

/Zuwena